KENYA KUWA MWENYEJI WA MSIMU WA PILI WA MASHINDANO YA COPA COCA –COLA KWA MATAIFA YA AFRIKA

Mashindano ya Pan-Afrika ni kuonesha ujuzi na vipaji lengo ni kuendeleza wachezaji vijana wa mpira kuwa kizazi kinachofuata cha nyota wa soka

Msimu wa pili wa kombe la Afrika la COPA Coca- Cola utafanyika mwaka huu Thika, Kenya kuanzia tarehe 2 mpaka 5 desemba 2019.

Wenyeji na mabingwa wa kwanza, Kenya watakuwa wakitafuta kutetea taji lao waliloshinda mwaka jana kwenye michezo iliofanyika Nakuru, Kenya.

Mwaka huu, mashindano ya COPA Coca- Cola yalikuwa ni Zaidi ya mpira wa miguu kwa shule zote zilizoshiriki barani Afrika. Imechangia kuleta mabadiliko ya tabia kwa kuanzisha ukusanyaji wa plastiki kama sehemu ya kuwaelimisha juu ya umuhimu wa mazingira safi kwa kutunza utupaji wa plastiki zilizotumika.

Kenya karibia kilogram 92, 057.50 zilikusanywa katika kipindi chote cha kuwani ubingwa na shule tano zililizokusanya idadi kubwa zilishinda ujenzi wauboreshaji wa viwanja sehemu ya kuchezea katika taasisi zao. Shule hizo ni Mutuini High kutoka Nairobi, St. Charles Lwanga Secondary School Kutoka Pwani, Mwiruti Mixed Secondary kutoka mkoa Rift and Mountain, Bishop Okul Girls kutoka mkoa wa Nyanza pamoja na Nyang'ori High School Western region.

Katika mashindano ya Pan-Afrika, timu kumi na mbili (12) zitashindana dhidi ya kila mmoja kuamua nani atakuwa bingwa wa chini ya miaka 16 wa Afrika. Timu zinazoshiriki ni pamoja na Uganda, Tanzania, Afrika Kusini, Zambia, Zimbabwe, Botswana, Angola, Ethiopia, Msumbiji, Burkina Faso, Namibia na nchi mwenyeji Kenya.

“Kombe la COPA Africa ni jukwaa ambalo litakwenda mbali zaidi katika kuhakikisha wanafunzi ndio kizazi kijacho cha nyota wa mpira wa miguu. Safu ya nyota ambao mashindano haya yamewatoa kwa timu za taifa kutoka kwenye timu zinazoshiriki ni ushahidi wa muhimu ya michezo hii.

Washirika wetu, Shirikisho la michezo kwa shule za sekondari Kenya (KSSSA) limeunga mkono sana na limeweza kuhakikisha mafanikio ya michezo” alisema Mr. Evanson Ndungu, Coca-Cola Meneja Masoko- Kenya, The Coca-Cola Company, Kenya.

Jumla ya mechi 20 zitachezwa kwa kipindi chote cha mashindano. Mfumo wa michezo utakuwa na timu kumi na mbili zilizogawanywa katika makundi manne. Kila kundi litakuwa na timu tatu. Timu mbili bora kila kundi zitaingia robo fainali. Kisha timu zitakutana kwa michezo ya mtoano mpaka timu bora itakaposhinda.

Classified - Confidential

Kampuni ya Coca-Cola inawawezesha watu ulimwenguni kote kupata uzoefu na kusherehekea mapenzi yao kwa mpira wa miguu. Kampuni ya Coca- Cola inaushirika wa muda mrefu zaidi na FIFA na uhusiano rasmi tangu 1974 na mdhamini rasmi wa Kombe la Dunia la FIFA ulionza mnamo 1978.

"Hapo awali, kampuni iliwekeza kwa kuchukua wachezaji bora na kuwapeleka katika mafunzo maalum kwenye kambi za kimataifa za COPA Coca-Cola ambapo walitembelea miji mingi ya kandanda. Sasa, tunawaweka wanafunzi kwenye mashindano ya kirafiki yanayoendeshwa kitaalam, Makocha wengi na wavumbuzi wa vipaji (Maskauti) kutoka kwenye vilabu bora pande zote za bara la Afrika watakuwa wakichagua vipaji na kuhakikisha wanaviendeleza katika safari yao ya mpira wa miguu.

Tunawasihi wadau wote wa mpira wa miguu, wazazi, walimu na maskauti waende pamoja nasi katika safari hii kugundua vipaji vya mpira wa miguu barani Afrika, " alisema Bi.Phillipine Mtikitiki – Meneja mkuu , Coca-Cola East & Central Africa Franchise

Michezo hiyo ni sehemu ya dhamira pana ya kampuni hiyo kuboresha michezo katika bara. Tangu 1989, mashindano ya COPA Coca-Cola yamekuwa yakichezwa barani Afrika kila mwaka na nchi ya kwanza kucheza michezo hiyo ilikuwa Zimbabwe. Hii ni kwa kuongeza uwekezaji wa kampuni hiyo kwenye Ziara ya Kombe la Dunia la FIFA kwa miaka kadhaa Kombe limekuwa likitembelea Zaidi ya nchi 50 ikiwemo Kenya kuleta Kombe la dunia karibu na watu.

Kuhusu kampuni ya Coca-Cola

Kampuni ya Coca-Cola (NYSE:KO) ni kampuni kubwa ya vinywaji duniani, inayozalisha zaidi ya chapa 500 kwa watu kwenye nchi zaidi ya 200.

Kwenye chapa zetu zenye thamani ya Dola Bilioni 21, chapa 19 ni bila sukari au kwa kiwango kidogo cha sukari kwa watu kuchagua kujipanga na matumizi yao ya sukari.

In addition to our namesake Coca-Cola drinks, some of our leading brands around the world include: Kwa kuongezea kwenye jina letu la vinywaji vya Coca-Cola, baadahi ya chapa zinazoongoza duniani ni kama: AdeS soy-based beverages, Ayataka green tea, Dasani waters, Del Valle juices na nectars, Fanta, Georgia coffee, Gold Peak teas na coffees, Honest Tea, Minute Maid juices, Powerade sports drinks, Simply juices, smartwater, Sprite, Vitaminwater, na Zico coconut water.

Coca-Cola ipo makini kuhusu kuleta mchango chanya duniani.

Hili linaanzia na kupunguza sukari kwenye vinywaji vyetu na kuendelea kuleta viburudisho vipya vyenye tija. Inaamaanisha pia muendelezo wa kupunguza athari za kimazingira, kutengeneza nafasi za vipaji kwa washirika wetu na kuleta fursa za uchumi popote tulipo. Kwa pamoja na washirika wetu wa viwandani, tumeajiri zaidi ya watu 700,000 duniani. Kwa maelezo zaidi, tembelea kurasa zetu za kidgitali kupitia www.coca-colacompany.com, kisha tufuate @The Coca-Cola Company kwenye Twitter, Instagram, Facebook na LinkedIn.